**MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI**
**(EWURA)**

**NAMBA YA MALALAMIKO: GA.71/135/LZ/2024/33**
**NAMBA YA LOIS: COMP-2025-00000009**

**KATI YA**

**KINANA MAULIDI SANGI ................................................................ MLALAMIKAJI**

**NA**

**SHIRIKA LA UMEME TANZANIA ............................................... MLALAMIKIWA**

---

**AMRI**

---

***(Imetolewa na Katibu wa Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA tarehe 10 mwezi Februari 2025)***

**MALALAMIKO HAYA** yameletwa mbele ya Katibu wa Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA kwa ajili ya kutoa uamuzi leo tarehe 10mwezi Februari 2025, kwa madai kwamba Mlalamikiwa arudishiwe uniti 138 zilizokuwemo kwenye dira yake namba 43002153856 ambayo ilibadilishwa na kuwekwa dira mpya namba 47003182806 nyumbani kwake Kirumba-Mlimani B, Wilaya ya Ilemela, Mkoa wa Mwanza.

Mlalamikaji anadai kuwa mnamo tarehe 8 Novemba 2024, mafundi wa Mlalamikiwa walibadilisha dira yake na kumfungia dira mpya wakati huo dira ilikua na uniti 138. Mlalamikaji anaendelea kueleza kwamba Mlalamikiwa aliahidi kuhamishia uniti hizo kwenye dira mpya lakini hakufanya hivyo. Hatimaye Mlalamikaji ameleta shauri lake EWURA ili aweze kupata haki yake.

Baada ya kupokea malalamiko tarehe 13 Disemba 2024, Mamlaka (EWURA) ilimwandikia Mlalamikiwa na kumuamuru kuwasilisha utetezi wake kwa maandishi ndani ya siku ishirini na moja (21) kwa mujibu wa Kanuni ya 6 (1) na 7 (1) ya Kanuni za EWURA za Utatuzi wa Migogoro - (EWURA (*Consumer Complaints Settlement Procedure), Rules 2020*)).

Mnamo tarehe 16 Januari 2024, Mlalamikiwa aliwasilisha utetezi wake na kukiri kupokea malalamiko ya Mlalamikaji na kwamba tayari amekwishatatua changamoto hiyo. Mlalamikiwa anaijulisha Mamlaka kwamba tayari amekwisha mrudishia uniti zote 138 kwenye dira yake Mlalamikaji namba 47003182806. Baada ya kupokea majibu hayo, Mamlaka ilimtafuta Mlalamikaji ili kudhibitisha kama ni kweli amepatiwa uniti zake. Tarehe 27 Januari Mlalamikaji alituma ujumbe kwa njia ya simu namba 0755 872 979 na kudhibitisha kwamba ni kweli Mlalamikiwa amekwishampatia uniti zake zote. Mlalamikaji ameishukuru Mamlaka kwa kuweza kumsaidia kutatua malalamiko yake na ameomba kuondoa malalamiko hayo dhidi ya Mlalamikiwa.

Katibu wa Bodi **ANATOA AMRI** kwamba malalamiko haya yaondolewe na kila upande utabeba gharama za uendeshaji wa malalamiko haya.

**IMETOLEWA KWA LAKIRI** ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) hapa Dodoma leo tarehe 10 mwezi Februari 2025.

..........................
**TONI S. MBILINYI**
**KATIBU WA BODI**